JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

# TAHADHARI KWA UMMA KUHUSU UGONJWA WA HOMA YA DENGUE HAPA NCHINI, ILIYOTOLEWA NA WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

**11 APRIL 2019**

**Ndugu Wanahabari na Wananchi,**

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, inatoa taarifa kwa umma kuhusu kuendelea kuwepo kwa ugonjwa wa homa ya Dengue hapa nchini. Ugonjwa huu umeibuka tena na kuendelea kuthibitishwa kuwepo hapa nchini hususani katika jiji la Dar es Salaam na Tanga kuanzia mwezi wa Januari 2019.

Hadi kufikia tarehe 2 Aprili 2019 kati ya watu 470 waliopimwa, wagonjwa **307** wamethibishwa kuwa na virusi au walikwishapata ugonjwa wa Dengue na kati ya hao **252** ni kutoka Dae Es Salaam na 55 ni kutoka Tanga. Katika jiji la Dar es salaam wagonjwa wamethibitishwa katika baadhi ya hospital zikiwemo Mwananyamala, Ilala, Temeke, Vijibweni, AghaKhan, Regency, IST, Ebrahim Haji na kutoka Mkoa wa Tanga katika hospital za Bombo, Agha Khan, Burhani Street 4 na Safi Medics.

**Ugonjwa wa Homa ya Dengue si mpya hapa nchini kwani umewahi kuripotiwa hapa nchini katika miaka ya 2010, 2013, 2014 na 2018.**

**Ndugu Wanahabari na Wananchi,**

Ugonjwa wa Homa ya Dengue unasababishwa na virusi vinavyoenezwa na mbu wa aina ya **Aedes** ambao ni weusi wenye madoadoa meupe yenye kungaa. **Dalili za ugonjwa** huu ni **homa ya ghafla, kuumwa na kichwa hususani sehemu za macho**, **maumivu ya viungo na uchovu.** Dalili hizi huanza kujitokeza kati siku ya 3 hadi 14 tangu mtu alipoambukizwa virusi vya homa ya Dengue. Wakati mwingine dalili za ugonjwa huu zinaweza kufanana sana na dalili za **Malaria,** hivyo basi wananchi wanaaswa kuwa makini pindi wapatapo homa, **wahakikishe wanakwenda kupata huduma kwa vituo vya kutolea huduma za afya** ili waweze kupimwa na kupatiwa tiba sahihi. Mara chache hutokea mgonjwa wa homa ya dengue **kutokwa na damu** sehemu za fizi, mdomoni, puani, kwenye macho na pia kwenye njia ya haja kubwa au ndogo.

**Ndugu Wanahabari na Wananchi,**

Virusi vya Homa ya Dengue vinaenezwa kwa binadamu baada ya kuumwa na mbu aina ya ***"Aedes"*** mwenye maambukizi ya virusi vya homa hiyo. Mbu hawa hupendelea kuzaliana kwenye maji yaliyotuama karibu na makazi ya watu au hata ndani ya nyumba. Viluwiluwi vya mbu hawa huweza kuishi katika mazingira ya ndani ya nyumba mpaka wakawa mbu kamili na kuanza kusambaza ugonjwa huu kwa binadamu. Mbu hawa huwa na tabia ya kuuma zaidi wakati wa mchana hasa wakati wa asubuhi jua linapochomoza na jioni jua linapozama.

Ugonjwa huu hauenezwi kutoka kwa binadamu mmoja kwenda kwa mwingine bila ya kuwepo na kuumwa na mbu mwenye vimelea. Hadi sasa hakuna chanjo ya homa ya Dengue nchini wala tiba ya moja kwa moja ya ugonjwa huu. **Mgonjwa mwenye homa ya dengue hutibiwa kutokana na dalili zitakazoambatana na ugonjwa huu kama vile homa, kupungukiwa maji au damu.** Mgonjwa mwenye dalili za homa ya Dengue anashauriwa kuwahi mapema kwenye kituo cha kutolea huduma za afya ili kupata huduma stahiki kwani endapo mgonjwa atachelewa kupatiwa huduma za matibabu anaweza kupoteza maisha.

**Ndugu Wanahabari na Wananchi,**
Wizara inaendelea kusisitiza jukumu la kila mmoja wetu kuhakikisha kuwa mazalio ya mbu yanaangamizwa na pia kujizuia kuumwa na mbu. Aidha Wizara inawasihi wananchi kuungana na Halmashauri pamoja na Mikoa katika juhudi za kupambana na kuthibiti kuenea kwa ugonjwa huu. Jamii izingatie kujilinda dhidi ya mbu ikiwa ni pamoja na;

**Kudhibiti na Kuangamiza mazalio ya mbu kwa**

1. Kufukia madimbwi ya maji yaliyotuama au kunyunyuzia dawa ya kuua viluwiluwi vya mbu kwenye madimbwi hayo
2. Kuondoa vitu vyote vinavyoweza kuweka mazalio ya mbu kama vile, vifuu vya nazi, makopo, magurudumu ya magari yaliyotupwa hovyo, nk.
3. Kufyeka vichaka vilivyo karibu na makazi ya watu
4. Kuhakikisha maua yanayopandwa kwenye makopo au ndoo hayaruhusu maji kutuama
5. Kufunika mashimo ya maji taka kwa mfuniko imara
6. Kusafisha gata za paa la nyumba ili kutoruhusu maji kutuama

**Kujikinga na kuumwa na mbu**

7. Kutumia dawa za kufukuza mbu "mosquito repellants"
8. Kuvaa nguo ndefu kujikinga na kuumwa na mbu
9. Kutumia vyandarua vyenye viuatilifu (hata kwa wale wanaolala majira ya mchana)
10. Kuweka nyavu kwenye madirisha na milango ya nyumba za kuishi

**Ndugu Wanahabari na Wananchi,**
Wizara pamoja na Mikoa na Halmashauri tunachukua hatua zifuatazo kufuatia uwepo wa ugonjwa huu hapa nchini;

1. Kupulizia dawa ya kuuwa mbu katika mazingira katika mkoa wa Dar Es Salaam
2. Kuendelea na kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji wa ugonjwa wa Dengue uliopo kwenye vituo maalum 'Sentinel Surveillance Sites' ambavyo vipo katika mikoa ya

Dar Es Salaam ambavyo ni katika hospitali za Mwanayamala, Ilala,Temeke na vijibweni na vile vile katika hosipitali ya Bombo katika mkoa wa Tanga.

3. Kuimarisha ufuatiliaji wa magonjwa nchi nzima kwa kutumia mfumo uliopo wa ukusanyaji wa taarifa, ambapo tunaendelea kupata taarifa za kila siku juu ya mwenendo wa ugonjwa huu na magonjwa mengine
4. Kuimarisha Utambuzi wa ugonjwa katika maabara ili kuweza kuthibitisha ugonjwa huu
5. Kuhimiza ufuatiliaji wa homa hii kwa mikoa yote hapa nchini
6. Kutoa elimu kwa jamii kupitia vyombo vya habari pamoja na ujumbe kwa njia ya mitandao ya kijamii.

**Hitimisho**

Wizara inaendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa ugonjwa huu wa Homa ya Dengue nchini. Aidha, wananchi wanashauriwa kutokuwa na hofu na kuwahi kwenda katika vituo vya kutolea huduma za afya mara waonapo dalili za ugonjwa huu kama nilivyoainisha. Jamii inashauriwa kuhakikisha kuwa mazalio yote ya mbu yanaangamizwa hasa kipindi hiki cha mvua. Wizara inaendelea kushirikiana na wadau wa sekta na mashirika mbalimbali kufuatilia na kudhibiti ugonjwa huu.

Imetolewa na

**Dkt. Faustine Ndugulile (Mb)**
**Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto**
**11 APRIL 2019**